*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA**
**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MUSOMA.**
**S.L.P 54 MUSOMA.**
**SIMU :0755 671818, 0767 082905,0752 525063**
**E-mail :musomatechsecondaryschool@gmail.com**

Ndugu ------------------------------------------------

S.L.P. ------------------------------------------------

----------------------------------------------------------

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA TANO 2024/2025**

1.0 Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa katika Shule hii, Kidato cha **Tano (2024/2025)** Mchepuo wa……….. Shule ya Musoma Sekondari ya Ufundi iko katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma Mkoani Mara, umbali wa Kilomita 4 kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. Kwa Kutokea Stendi kuu ya Mabasi ya Bweri, barabara iendayo Musoma Mjini ni umbali wa kilomita 5,Gharama za Usafiri ni Tsh 2000 kwa usafiri wa BODABODA na kiasi cha Tsh 1000 kwa usafiri wa Bajaji kuna kibao kinachoitambulisha shule upande wa kushoto ukiwa unatokea Bweri Stand kuelekea Musoma Mjini.

2.0 Shule itafunguliwa Muhula wa kwanza tarehe **01/07/2024.** Muda wa kuripoti ni kuanzia **saa 02:00 Asubuhi** hadi **saa 12:30 jioni.** Mwanafunzi anatakiwa kuwa ameripoti shuleni kuanzia tarehe ya kufungua na mwisho wa **kuripoti itakuwa wiki mbili tokea tarehe ya kuripoti**. Mara mwanafunzi afikapo shuleni **aripoti Ofisini kwa Makamu Mkuu wa Shule kwa mapokezi na usajili.** Makamu Mkuu wa shule atahakikisha kwamba mwanafunzi amekuja na hati ya malipo "Pay in Slip" inaonesha kuwa mwanfunzi amelipia michango ya uendeshaji kwenye **Akaunti za Shule zilizoko katika Benki ya NMB kama ifuatavyo;** fedha za michango ya shule zilipwe kwenye **Akaunti Namba 30301100043 yenye jina MUSOMA TECHNICAL.**

**3.0 Mwanafunzi ajapo shuleni ni muhimu aje na vitu vifuatavyo;**

i. Kivuli cha Cheti cha Kuzaliwa kinachotolewa na Serikali
ii. Fomu iliyojazwa na Daktari kuhusu Afya ya Mwanafunzi (Medical Examination Form).
iii. Fomu iliyojazwa ya maelezo binafsi ya mwanafunzi (Personal Particularas Form).
iv. Fomu ya kukubali masharti ya shule. Wewe na mwanao muisome kwa kina pamoja na sheria za shule mkizikubali, msaini fomu hizo na ziwasilishwe shuleni hapa wakati wa kuripoti.
v. Kivuli cha Cheti cha Matokeo na cheti cha kumaliza Kidato cha Nne (Leaving Certificate).
vi. **Picha nne (04) "Passport Size" za Mwanafunzi na Picha moja moja "Passport Size" za Wazazi na ndugu wa karibu wa Mwanafunzi wanaoweza kumtembelea Mwanafunzi au kuitwa wakati wa Matatizo mbalimbali pamoja na namba zao za Simu.**

4.0 Ndugu Mzazi/Mlezi, Shule hii haina utaratibu wa chakula maalum (Special diet) kwa mwanafunzi mmoja

mmoja tofauti na kile kinachoandaliwa kwa ajili ya wanafunzi wote. Vile vile shule ina mihula miwili (02) ya masomo na kila muhula unapokwisha shule huwa inafungwa. Hivyo mzazi unatakiwa kumtumia mwanao nauli ya kurudi nyumbani kwa ajili ya mapumziko. Shule hairuhusu mwanafunzi kubaki shuleni wakati wa likizo. Pamoja na barua hii naambatanisha orodha kamili ya vifaa vya lazima mwanafunzi anavyopaswa kuja navyo na fomu mbili anazotakiwa kujaza na kuja nazo wakati wa kuripoti shuleni.

**MAGITA GABRIEL NYANGORE**
**MKUU WA SHULE**

## 5.0 VIFAA/MAHITAJI YA LAZIMA UNAYOTAKIWA KULETA:

**Michango.**

[i] Mchango wa uendeshaji wa Shule T.Shs.65,000/= kwa mwaka

[ii] Kitambulisho, Tahadhari, na Nembo Tsh.15000.

NB: Malipo yote yafanyike kupitia Akaunti yetu ya Bank NMB 30301100043
MUSOMA TECH .S.S

**SARE YA SHULE. Sare ya shule hii ni**;

- Mashati mawili meupe yenye **mikono Mirefu**.
- Suruali mbili nyeusi zenye mifuko miwili ya pembeni na mmoja nyuma kulia zisizobana na zisiwe **"Jeans"** wala **"Modo"** Upana wa chini usipungue **inchi "15" ukipungua hiyo suruali haitakubaliwa.**
- **Tshirt mbili (2) za kushindia baada ya masomo rangi ya blue zenye kola nyeusi (Kwa mzazi atakayependa kununa shuleni zinapatikana kwenye maduka yaliyo karibu na shuleni kwa Tsh 12,000 kila moja zikiwa na nembo ya shule).**
- Viat,u vya ngozi vyeusi vya kamba jozi 2 visiwe na kisigino kirefu wala shingo ndefu. Soksi jozi 2 rangi nyeusi.
- Sweta ya rangi ya kijani kibichi (Rangi ya mimea) yenye alama ya "V" shingoni. (**Kwa mzazi atakayependa kununa shulen zinapatikana maeneo ya shule kwa Tsh 12,000/=)** Suruali ya rangi ya damu ya Mzee– huvaliwa baada ya saa za masomo.
- Aje na viatu na nguo za michezo. Bukta, Tshirt ya rangi ya Blue na track za rangi ya blue (zinapatikana karibu na shule)
- Track suit rangi ya blue (zinapatikana karibu na shule zikiwa na nembo ya shule
- Mkanda wa ngozi rangi nyeusi au ugolo wa ukubwa wa kati usio na "bicross" kubwa.
- Tai moja rangi ya bluu yenye mistari myeupe (zinapatikana karibu na shule zikiwa na nembo ya shule) **MUHIMU: Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuwa na nguo za nyumbani shuleni.**

## 6.0 VIFAA VYAKE BINAFSI VYA KUTUMIA BWENINI

- Godoro la "Sponge" la 2.5ft x6''x6" (unene ni nchi 6) hakikisha unaleta godoro lililoagizwa kwa size hiyo **(Zinapatikana maeneo ya shule endapo utashindwa kupata huko uliko zingatia vipimo).**
- Shuka mbili mpya rangi moja ya bluu bahari (Light blue).
- Mto na foronya ya rangi ya blue bahari.
- Chandarua (Vitanda vyetu ni Futi 2.5)
- Ndala/Kandambili
- Taulo
- Sanduku la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake ni (lazima)
- Ndoo moja ya kuchotea maji na dumu la lita 5 kwa ajili ya kutunzia maji yake ya kunywa (Lazima).
- Mwanafunzi aje na Toilet paper walau 10 kwa matumizi yake.
- Sahani, bakuli, Kijiko na Kikombe cha nusu lita .
- Fedha za matumizi yake muhimu ya kila siku na nauli ya kurudi nyumbani wakati wa likizo au dharura.

**VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI NA WAKATI WA MITIHANI**

1. Ream ya Karatasi A4 mbili(**AINA YA DOUBLE "A" (Ni lazima kila mwaka).**
2. Mathematical set 3.Kamusi (English Dictionary)
4. Madaftari makubwa (Counter Books) yasiyopungua 08. Scientific calculator ya " function kuanzia fx – 82MS to fx –991MS (Kwa Kidato cha Tano michepuo ya **PCM, PGM, EGM,CBG,PCB na HGE). (Zinapatikana maeneo ya shule endapo utashindwa kupata huko uliko).** Dissecting Kit" (Kwa wanafunzi wanao soma Biology )

## A. KILA MWANAFUNZI WA SHULE HII NI LAZIMA AZINGATIE MAMBO YAFUATAYO;

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi,wanafuzi wenzake wote na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Kuhudhuria katika kila shughuli ndani na nje ya shule pale unapohitajika.
c) Kuhudhuria bila kukosa kwenye maandalio ya usiku (Night Preparation & Morning preparation).
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuepuka kuwa nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.
e) Kutunza usafi na mazigira ya shule wakati wote.
f) Kuvaa sare ya shule wakati wote mwanafunzi anapokuwa nje ya shule na nje ya shule. g) Kufuata ratiba ya shule wakati wote.

## B. MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA

a) Kuvuta sigara.
b) Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu na ndevu.
c) Kuvaa mavazi yasiyo sare rasmi ya shule ndani ya eneo la shule na nje ya shule.
d) Kupigana/ kuchochea ugomvi au kumpiga mtu yeyote.
e) Kuiga mitindo ya kihuni isiyofaa katika jamii.
f) Kwenda nje ya shule bila ruhusa kutoka kwa mwalimu.
g) Kumiliki simu shuleni.
h) Kula chakula nje ya Bwalo la chakula bila ruhusa.
i) Kupeleka mgeni Bwenini ama sehemu nyingine isiyohusika tofauti na maeneo yaliyoelekezwa.
j) Kwenda kwenye yumba za walimu ama watumishi wasio walimu bila ruhusa au sababu ya muhimu.
k) Kuingia au kutembelea maeneo ya kuuzia vileo na majumba ya starehe.

## C: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI:

1. Wizi
2. **Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/Utoro.**
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
4. Kutoa lugha chafu kwa Wanafunzi wenzake, Walimu/Walezi na Jamii kwa ujumla.
5. Kupigana Mwanafunzi kwa Mwanafunzi,kumpiga Mwalimu au mtu yeyote Yule.
6. Kusuka/Kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika.Wanafunzi wakati wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo Shuleni.
7. Kufuga ndevu.
8. Ulevi au unywaji wa Pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
9. Uvutaji wa Sigara.
10. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
11. Kushiriki matendo ya uhalifu, Siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
12. Kusababisha Mimba au kumpa mimba msichana.
13. Kudharau bendera ya Taifa.
14. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
15. Uharibifu wa Mali ya Umma kwa makusudi.
16. **Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi; kukutwa na “line” ya simu, “charger” au betri ya simu katika mazingira ya Shule.**

**ZINGATIA: MWANAFUNZI ATAKAYEPATIKANA NA SIMU SHULENI ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA NA KULIPA FAINI YA TSH.200, 000/=**.

**PIA SHULE YETU KWA SASA IMEFANYIWA UKARABATI MKUBWA NA SERIKALI.HIVYO MWANAFUNZI AKIJIHUSISHA NA UHARIBIFU WA MALI YA UMMA IKIWEMO KUCHAFUA KUTA KWA MAANDISHI,KUVUNJA TAA,VIOO,MILANGO N.K ATALAZIMIKA KUFIDIA GHARAMA ZA UHARIBIFU HUO.**

**MKUU WA SHULE**

*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## SHERIA ZA MAHUSUSI ZA SHULE NA MALEZI BORA SHULENI

Wanafunzi wote mnakumbushwa kuzingatia sheria na taratibu zote za malezi bora unapokuwa hapa shuleni na nje ya shule kama zilivyoorodheshwa hapa juu,

**1. R A T I B A:**

Ratiba ya Shule ni Msingi wa mafanikio kwa kila mwanafunzi hivyo kila mwanafunzi anapaswa kuzingatia ratiba ya Shule kadri itakavyo tolewa kwa kila siku bila kukengeuka.

**2. U T I I:**

Mwanafunzi yoyote anapaswa awatii watu wote, amri na sheria zote ipasavyo kwa upesi bila ubishi, kusita wala kukawia pasipo manung'uniko yoyote.

Maswali yakiwepo ni baada ya kutii kufanyika. Ukosefu wa **utii** ni kosa kubwa sana la kinidhamu hapa Shuleni.

Mwanafunzi yeyote inabidi aheshimu bendera ya Serikali, Wimbo wa Taifa au wa Shule (Simama kila unapoimbwa). Nembo ya Taifa, Kiongozi wa Taifa na Fedha za Taifa.

**3.0 A D A B U N J E M A:**

[i] Adabu ni alama ya msingi wa heshima. Hivyo inampasa kila mwanafunzi aonyeshe adabu njema popote alipo na kwa wakati wote. Maneno na vitendo viovu hayatasita kuadhibiwa.

[ii] Wanafunzi wote wajiheshimu na kuwaheshimu watu wote bila ubaguzi.

[iii] Walimu husalimiwa 'Good morning/Afternoon/Evening Sir or Madam' kwa adabu. Watu wote wengine husalimiwa shikamoo.

[iv] Unapaswa kuitika ishara yeyote ya kuitwa na kukimbia kila unapoitwa.

**4.0 M I P A K A Y A S H U L E:**

Kila mwanafunzi anatakiwa kubaki katika eneo la shule wakati wote wa masomo na endapo itabidi kutoka nje ya eneo la shule lazima uwe na kibali (pass).
Adhabu ya kutoroka shule ni kusimamishwa au kufukuzwa shule.

**5.0 K E L E L E:**

Hii ni alama ya malezi mabaya. Watoto waliolelewa vizuri huwa na kauli na tabia nzuri za mawasiliano.
Hivyo ni marufuku kufanya aina yeyote ya ghasia au kelele au usumbufu wowote darasani, maktaba, maabara n.k. Ukibainika utachukuliwa hatua za kinidhamu.

**6.0 USAFI WA MAZINGIRA YA SHULE PAMOJA NA USAFI BINAFSI:**

[i] Ni marufuku kuchafua au kuziba vyoo au kuharibu miundo mbnu ya vyoo.
[ii] Ni marufuku kutupa aina yoyote ya uchafu mfano: makopo,

makaratasi kwenye maeneo ya shule.

[iii] Madarasa, varanda, vyoo, maabara vyote vifanyiwe usafi asubuhi na baada ya masomo na wahusika.

[iv] Ni mwiko kabisa kwa mwanafunzi kufanya yafuatayo:-

- Kuwa na nywele ndefu .
- Kunyoa nywele zote (Kipara).
- Kunyoa mitindo isiyofaa (denge, punk n.k.)
- Kufuga kucha, ndevu n.k.
- Kuvaa mavazi yasiyo na heshima na haswa kupunguza urefu au upana suruali (modo- zinazobana).
- Kuongeza mapambo ya aina yoyote juu ya sare ya shule kama vile:-
- Kuvaa makoti na majakets
- Kuvaa culture, chain n.k.

**0.7 M I C H E Z O:**

Kwa kuwa michezo ni sehemu ya malezi kila mwanafunzi anatakiwa ajiunge kwenye mchezo. Mwanafunzi asiyeshiriki michezoni ana mwelekeo mbaya na uhusiano na wenzake una kasoro.

**8.0 UTUNZAJI NA MATUMIZI YA MALI YA UMMA**:

[i] Mali yote ya shule ni mali ya umma. Haina budi itumiwe na kuitunza ipasavyo ili iweze kutumika kwako na wengine wanaokuja.

[ii] Wanafunzi wote lazima waangalie na kutunza mali na vifaa vyote vya shule vikiwepo vitabu, viti, madawati, meza, bomba za maji, vifaa vya umeme, milango, madirisha vifaa vya usafi n.k.

[iii] Hapana budi kurudisha vifaa vyote ulivyoazima ama kukabidhiwa wakati unapohitajika kufanya hivyo. Kuiba, kupoteza, kuharibu, kuchezea au kuzembea mali ya Serikali ni uhalifu mkubwa; adhabu yake ni kulipishwa mali nyingine, kufukuzwa shule, na au kushitakiwa mahakamani.

[iv] Ni marufuku kuchora, kuandika maandishi ya aina yoyote ukutani, kwenye madawati, viti, malangoni, au sehemu yeyote ile. Adhabu kali itatolewa ikiwa ni pamoja na kupaka rangi au kununua upya kifaa husika.

**9.0 MALI BINAFSI YA MWANAFUNZI:**

[i] Kutokutunza mali yako mwenyewe ni **UZEMBE.** Ni muhimu kutokuwa na mali za anasa kama vile camera, simu, walkman, simu ya mkononi haziruhusiwi kabisa. Ukikamatwa navyo hutarudishiwa na adhabu itafuata ikiwemo kufukuzwa Shule.

10. **KUTUNZA AMANI NA KUIDUMISHA**:

[i] Ni marufuku kuchokoza, kuonea, kutukana, kudharau, kutania, kusengenya pia kuumiza mtu yeyote,kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k . Ukiwa na shida peleka shauri lako kwa viongozi wahusika nao watakutafutia haki yako. Pia kuna vikao mbalimbali vya shule tayari kukusaidia wakati wote. Kumumiza mwenzako makusudi, **kupigana** ni kosa la kukufukuza shule au kushtakiwa mahakamani.

[ii] Ni marufuku kufanya mikutano ya siri. Ukibainika utafukuzwa shule moja kwa moja.

[iii] Ni marufuku kufanya fujo yoyote au mgomo. Ukibainika utafukuzwa shule au kushtakiwa mahakamani.

**11. U L E V I N A U A S H E R A T I:**

[i] Kuonja kileo cha aina yoyote ni marufuku popote pale ulipo na kwa wakati wote,pia

hauruhusiwi kutembelea majumba ya starehe wala nyumba za kulala wageni. Ukibainika utafukuzwa shule moja kwa moja au kusimamishwa masomo.

[ii] Ni marufuku kabisa kwa mwanafunzi kuvuta sigara, bangi, madawa ya kulevya. Aidha kuvuta bangi na utumiaji wa madawa ya kulevya ni **MARUFUKU KABISA**. Ukibainika utafukuzwa shule na kushtakiwa mahakamani.

**[iii]** Uhusiano wowote wa kimapenzi kati ya mvulana na msichana walio wanafunzi – au watu wa mtaani hautavumiliwa kabisa. Hivyo basi, aina zote za uasherati litapelekea **KUFUKUZWA SHULE NA KUSHTAKIWA MAHAKAMANI.**

**12. W A G E N I:**

Ni marufuku kupokea wageni wa aina yeyote wakati wa masomo bila ruhusa ya mwalimu wa zamu.

**13. D I N I N A I M A N I:**

[i] Kipindi cha dini ni kama vipindi vingine, lazima mwanafunzi aingie na kutimiza sheria zote katika dhehebu lake.

[ii] Vipindi vya dini na ibada zote ni lazima zifuatwe barabara kwa wakati wake.

[iii] Ni wajibu kuheshimu dini na imani za watu wote.

[iv] Shughuli za kidini haziingiliani na muda wa kawaida wa masomo.

**[v]** Waalimu watakaofika shuleni kufundisha vipindi vya **DINI** watambulishwe Ofisi ya Mkuu wa Shule.

**14. E L I M U Y A K U J I T E G E M E A:**

Kufanya kazi ni jambo la lazima na siyo hiari. Kuchelewa , kutega, uvivu na ujeuri kwenye kazi, yote haya ni uhalifu mkubwa na utaadhibiwa. Usipokoma utasimamishwa masomo.

FOMU: **NAMBA 1**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI KATIKA KIDATO CHA -------------------**

**MWAKA --------------------**

***(Fomu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi pamoja na Mwanafunzi)***

Fomu hii ijazwe na mzazi/Mlezi pamoja na Mwanafunzi aliyechaguliwa kuingia/Kuhamia kidato cha ---------------------------------------- kasha mwanafunzi ailete shuleni (**Ithibitishwe na Mwenyekiti/Mjumbe wa Kijiji/eneo unaloishi**)

1. Mimi ---------------------------------------------(Jina la mwanafunzi) kwa hiari yangu, ninakubali/sikubali nafasi niliyopewa ya kuingia Kidato cha ------------------------- katika Shule ya Sekondari Musoma. Nitakuwa tayari kuzifuata sheria zote za shule wakati wote niwapo shuleni. Kuvunja sheria ya shule kwa makusudi itakuwa nimekiuka ahadi hii ninayotoa na nitastahili kuchukuliwa hatua za kinidhamu zinazostahili hata kufukuzwa shule.

--------------------

(Sahihi ya Mwanafunzi)
Tarehe ..............................

2. Mimi..........................................................(Jina la Mzazi/Mlezi) wa .......................................... ----------------

   Nakubali/sikubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda wote awapo shuleni analazimika kufuata sheria za shule na kuwa mtiifu kwa walezi wake.Pia nakubali/sikubali kulipa ada,michango na maelekezo mengine yatakayotolewa shuleni.

--------------------

(Sahihi ya Mzazi/Mlezi)
Namba ya simu...................................

Tarehe ..............................

3. Mimi ------------------------------------(Jina la mwenyekiti wa mtaa) ninathibitisha kuwa Ndugu ------------------------------ ni Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu aliyechaguliwa kuingia Kidato cha Tano ni mkazi wa kata ya -----------------------------------------------------.

4. Namba ya simu ya Mlezi (i)..........................................................................

-----------------------------

(Sahihi ya Mwenyekiti/Mjumbe)
Tarehe ..............................................

*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**FOMU YA UTII NA TABIA NJEMA NA KUKUBALI NAFASI**

Mimi.......................................................................................................-................(jina kamili)

Kidato cha..................................................................mwaka ..................................................

Natambua wajibu wangu kwa Taifa kama mwanafuni na naahidi:-

(a) Kwamba nitatii na kuwaheshimu viongozi wangu wote kuanzia ngazi ya mamoniter, viranja, walimu, watumishi wote hadi Mkuu wa Shule.

(b) Kwamba nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.

(c) Kwamba sitatoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo na usio wa masomo labda tu kwa shughuli maalumu na baada ya kupata kibali maalumu kutoka kwa Mwalimu au Mkuu wa Shule mwenyewe.

(d) Sitagoma wala kusababisha mgomo shuleni.

(e) Kwamba kama nitashindwa kufuata hayo yote hapo juu, hatua kali ichukuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule.

Tarehe .......................................................... - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - -

Jina na Sahihi ya Mwanafunzi

Tarehe .......................................................... ..................................................................

Jina na Sahihi ya Shahidi Mzazi/Mlezi

Tarehe .......................................................... - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - -

Sahihi ya Mkuu wa Shule

**FOMU: NAMBA 3**

**SHULE YA SEKONDARI MUSOMA FOMU**

**YA KUJIANDIKISHA SHULENI <u>HABARI</u>**

**<u>ZA MWANAFUNZI</u>**

1. Jina kamili (Kama kwenye mtihani) -----------------------------------------------------
2. Tarehe ya kuzaliwa.................................................Dini ............................................
3. Mahali na Wilaya ulipozaliwa ....................................................................................
4. Kata anayoishi kwa sasa...............................................................................................
5. Shule ulipomaliza,Kidato ..................................................................
6. Kidato unachokuja kuingia hapa shuleni -------------------------------------------------
7. Majina ya vyama vya masomo uliyowahi kujiunga:

   (i) ..........................................................................................................
   (ii) ..........................................................................................................
   (iii) ....................................................................----------------------------------------

8. Michezo/Masomo unayopendelea:

   (i) ..........................................................................................................
   (ii) ..........................................................................................................-------
   (iii) ..........................................................................................................

9. Kazi yeyote ya uongozi uliyowahi kufanya kama vile kiongozi wa michezo, kwaya, ngoma, kiranja, maktaba n.k.

| **Madaraka/Uongozi** | **Shule/Mahali** | **Mwaka** |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |

9. Mambo unayopendelea kufanya nje ya masomo (k.m. m ichezo, ushonaji n.k.)

   (i) ..........................................................................................................
   (ii) ..........................................................................................................
   (iii) ..........................................................................................................

Tarehe:.............................. ------------------------------

Jina na Sahihi ya Mwanafunzi

**FOMU:NAMBA 4**

## SHULE YA SEKONDARI MUSOMA UFUNDI

## FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI

### HABARI ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Baba ..........................................................................
2. Kazi yake ..........................................................................
3. Jina kamili la Mama ..........................................................................
4. Kazi yake ....................------..........................................................
5. Jina kamili la Mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake)
 - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - -
6. Kazi na Anwani ya Mlezi ..........................................................................
 - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - -

7. Nyumbani kwa baba (alipozaliwa mtoto) ----------------------------------------------
 Kijiji/Mtaa............................................Wilaya............................................
 Kata............................................Mkoa............................................
 Tarafa ............................................

8. Anwani ya mahali pa kazi ya baba ..........................................................................
 - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - -

 Nambari ya simu..........................................................................-
9. Anwani ya mahali pa kazi ya mama ----------------------------------------------------
 Nambari ya simu ..........................................................................
10. Mtoto anaishi na (i) Baba tu (ii) Mama tu (iii) Wazazi wote (iv) Walezi **Kata isiyohusika***
11. Dini ya Baba............................................Dhehebu ..............................
 Dini ya Mama............................................Dhehebu ..............................
 Dhehebu unalotaka mwanao alelewe ..........................................................
12. Anwani kamili ya nyumba ambapo mtoto atakuwa nakwenda siku za likizo: --
 - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - -

13. Mimi............................................(Baba/Mama/Mlezi wa ..............................
 ............................................ Nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na haahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Tarehe............................................ ............................................
Jina na sahihi ya Mzazi/Mlezi

BANDIKA PICHA ZA WAZAZI/WALEZI HAPA CHINI KISHA ANDIKA UHUSIANO CHINI YA PICHA

**FOMU: NAMBA 5**

## MEDICAL EXAMINATION

To be completed by Medical Officer in Government Hospital in respect of all new entrants to Musoma Secondary School.

Full Name: ..........................................................................................................

Age: ..........................................................................................................

1. Chest : ..........................................................................................................
2. Blood count (Red and White) ..........................................................................................................
3. Urine Examination ..........................................................................................................
4. Stool Examination ..........................................................................................................
5. Syphilis Test ..........................................................................................................
6. T.B. Test ..........................................................................................................
7. Ear Test ..
8. Eye Test ..
9. Spleen ..........................................................................................................
10. Abdomen ..........................................................................................................
11. Addition information of any other physical, mental hereditary of infectious diseases:

    ----------------------------------------------------------------------------------------------------

    ----------------------------------------------------------------------------------------------------

    Treatment after examination ..........................................................................................................

    ----------------------------------------------------------------------------------------------------

**(Please state nature of treatment)**

**MEDICAL CERTIFICATE:**

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue further education.

Signature ..........................................................................................................

Designation..........................................................................................................

Station: ..........................................................................................................

Date..........................................................................................................

Official St

**VIFAA VYA USAFI ANAVYOPASWA KUNUNUA MWANAFUNZI KULINGANA NA TAHASUSI ALIYOCHAGULIWA.**

| **Na.** | **TAHASUSI** | **JINA LA KIFAA.** | **IDADI** |
|---|---|---|---|
| **1** | **PCM** | **JEMBE LENYE MPINI** | **01** |
| | | **SOFT BROOM** | **01** |
| | | **CHELEWA** | **01** |
| **2** | **PGM** | **SABUNI YA CHOONI LITA 5** | **01** |
| | | **FAGIO LA CHELEWA** | **01** |
| | | **SOFT BROOM** | **01** |
| **3** | **CBG** | **JEMBE LENYE MPINI** | **01** |
| | | **TOILET BROOM** | **01** |
| | | **CHELEWA** | **01** |
| **4** | **EGM** | **JEMBE LENYE MPINI** | **01** |
| | | **HARD BROOM** | **01** |
| | | **CHELEWA** | **01** |
| **5** | **HGE** | **SABUNI YA CHOONI LITA 5** | 01 |
| | | **HARD BROOM** | **01** |
| | | **MIFAGIO YA BUIBUI** | **01** |
| **6** | **HGK** | **JEMBE** LENYE MPINI | **01** |
| | | **SQUIZER** | **01** |
| | | **CHELEWA** | |
| **7** | **HGL** | **JEMBE LENYE MPINI**<br>**SOFT BROOM**<br>**SQUIZER** | **01** |

**Vifaa hivi vinapatikana karibu na Shule.**

**MAWASILIANO KWA USAIDIZI KAMA UTAHITAJI.**

**MKUU WA SHULE :** 0755671818/0712658280

MAKAMU 1 : 0752525063

MAKAMU 2; 0767082905

MTAALUMA : 0763961130

NIDHAMU ; 0683310919